WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI KABALE – BARIADI
S.L.P. 393 – BARIADI.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

UTANGULIZI:
Kama ilivyo kawaida kwa jumuiya ya watu wanaoishi pamoja ni lazima kuwepo na sheria na kanuni za kuwaongoza watu katika jumuiya hiyo ili waishi kwa amani na kuwa na ushirikiano mzuri katika kutekeleza malengo yote yanayoleta maendeleo. Hivyo sheria, kanuni na taratibu hizo zitamwezesha mwanafunzi kustawi kitaaluma na kuishi kwa amani na wanafunzi wenzake, walimu pamoja na wafanyakazi wengine wasio walimu na jumuiya yote inayoizunguka shule.

ZIFUATAZO NI SHERIA ZA SHULE

A. HESHIMA:

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ajiheshimu mwenyewe, awaheshimu wenzake, viongozi wa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wasio walimu na watu wengine wote wakubwa kwa wadogo.
2. Mwanafunzi anatakiwa asimame na kumsalimia mwalimu, mfanyakazi asiye mwalimu na mtu yeyote anayestahili kufanyiwa hivyo.
3. Ni marufuku kwa mwanafunzi kufanya mambo yafuatayo:-
   i. Kugombana au kupigana.
   ii. Kuandika au kutamka lugha chafu mahali popote pale.
   iii. Kuzua au kueneza taarifa za uongo.
   iv. Kuiba vifaa au kifaa cha shule au mtu mwingine.
   v. Kufanya vikao au mikutano shuleni bila kibali cha mkuu wa shule.
   vi. Kufanya mgomo wa aina yoyote.
   vii. Kutembelea kwenye vilabu vya pombe au majumba ya kufikia wageni [Guest House].
   viii. Kutumia pombe ya aina yoyote, madawa ya kulevya, kuvuta sigara au bangi.
   ix. Kupokea mgeni bila ruhusa ya mwalimu wa zamu.
4. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bender ya Taifa, Picha za Viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
5. Mwanafunzi anatakiwa anyooshe mkono juu na asimame anapoomba kuuliza au kujibu maswali darasani au kwenye mikutano.
6. Mwanafunzi anapoandika barua yoyote ya kiofisi inayokwenda nje ya shule, sharti barua hiyo ipitie kwa mkuu wa shule.
7. Mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya darasani, asitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi mwingine aliyeko.
8. Uhusiano kati ya mwanafunzi wa kike na wa kiume uwe wa kaka na dada. Pia uhusiano kati ya mwanafunzi na mwalimu au mfanyakazi uwe wa baba na binti yake au mama na mtoto wake. Uhusiano wa KIMAPENZI hauruhusiwi.

HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA
SHULE YA SEKONDARI KABALE BARIADI
FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

SHULE YA SECONDARI KABALE BARIADI,
SLP 393,
BARIADI,
15/12/2020.

KUMBUKUMBU NA KBSS/VOL III/2021.
JINA LA MWANAFUNZI.....
SLP.....
ITILIMA

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI
SHULE YA SEKONDARI KABALE-BARIADI

1.Ninayo furaha ya kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Kabale-Bariadi ambayo nimiongonimwa shule bora katika halmashauriya wilayaya Itilimana mkoa wa Simiyu. Hongerasana mhurawa kwanza wamasomo utanzarasmi 11/01/2021unatakiwakufikashulenisikuhiyobilakukosatayarikwaajiliyakuanzamasomo

2.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A.SARE ZA SHULE

(i) WAVULANA

(a) suruarijozimbili, suruariya kwanza rangiyadamu yam zee nayapiliranginyeusi
(b) Shatinyeupemikonomifupi
(c) Viatuvyeusivyakamba
(d) Soksinyeusi

B. WASICHANA

(a) Siketijozimbilimojayenyerangiyadamu yam zee nanyingine nyeusi yenye michirizi miwili myeupe upande wa mbele
(b) Shati (blauzi) nyeupe yenye mikono mifupi
(c) Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi
(d) Soksi nyeupe

03. MAHITAJI MENGINE KWA MWANAFUNZI

Madaftari makubwa tisa (9) kwaajiliya masomo ya Civics, Basic mathematics, Kiswahili, kingereza, Biology, Chemistry, History, Physics na Geography
Mathematical set, kalamuya wino mweusi au blue na penseli
Begi la kubebea madaftari

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KABALE BARIADI

.....

THE HEADMASTER
KABALE-BARIADI SEC. SCHOOL
ITILIMA.

FARAJA RAPHAELI MAGOTI

KWA MAWASILIANO ZAIDI TUMIA NAMBA ZIFUATAZO

0756375836 AU 0787570924

B. MAHUDHURIO:

1. Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni kila siku ya masomo au hata wakati wa likizo ikiwa atapangiwa kufanya hivyo.
2. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria kazi zote za mikono kama alivyopangiwa.
3. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
4. Mwanafunzi anatakiwa kutii kengele ya shule mara moja na kusimama katika mistari ya paredi.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama Baraza la shule, Ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera, mjadala [debate].
6. Mwanafunzi asipohudhuria shuleni kwa muda wa siku tisini [90] mfululizo atakuwa amejifukuza shule mwenyewe.
7. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutofika shuleni bila taarifa ya maandishi toka kwa mzazi wake.

C. KUWAHI:

i. Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni siku ya kufungua shule.
ii. Mwanafunzi anatakiwa kufika mara moja anapoitwa na kiongozi anayehusika, mwanafunzi, mwalimu, mfanyakazi au mtu yeyote aliyemwita.
iii. Mwanafunzi anatakiwa afike shuleni katika muda uliopangwa na awahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku au kama atakavyoelekezwa na mwalimu au kiongozi anayehusika.
iv. Mwanafunzi anatakiwa kuacha mara moja kazi anayoifanya kwenda haraka kwenye sehemu anayohitajika kama kuna jambo la dharura linalotokea.
v. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi kufika shuleni asubuhi na kuwahi kurudi nyumbani jioni.

D. SARE ZA SHULE:

i. Mwanafunzi anapotoka shuleni kwenda nyumbani au toka nyumbani kwenda shuleni anatakiwa awe kwenye sare ya shule.
ii. Mwanafunzi anatakiwa kuchomekea shati lake la shule popote pale akiwa kwenye sare ya shule.
iii. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa sare za shule kwa kuchanganya na mavazi mengine ya nyumbani anapokuwa katika shughuli za kishule.
iv. Hairuhusiwi kuvaliana sare za shule wala kuazimisha sare za shule kwa watu wengine mtaani.
v. Sare za shule zivaliwe kama ifuatavyo:-

a. Wavulana:

- Suruali rangi ya damu ya mzee na shati jeupe mikono mifupi zivaliwe siku ya jumatatu na jumanne.
- T.shirt rangi ya damu ya mzee na suruali rangi ya damu ya mzee zivaliwe siku ya jumatano.
- Suruali rangi nyeusi na shati jeupe mikono mifupi zivaliwe siku ya alhamis na ijumaa.

2. **Wasichana:**
   - sketi rangi ya damu ya mzee na shati jeupe mikono mifupi zivaliwe siku ya jumatatu na jumanne.
   - T.shirt rangi ya damu ya mzee na sketi rangi ya damu ya mzee zivaliwe siku ya jumatano.
   - Sketi rangi nyeusi na shati jeupe mikono mifupi zivaliwe siku ya alhamis na ijumaa.

vi. Mwanafunzi anapotakiwa kurudi shuleni muda wa jioni anatakiwa avae T.shirt pamoja na suruali au sketi inayohusika kwa siku hiyo.

E. USAFI:

i. Mwanafunzi anatakiwa awe msafi wa mwili na mavazi kila siku.
ii. Nywele zikatwe ziwe fupi na zichanwe kila siku, hairuhusiwi kusuka.
iii. Viatu ving'arishwe kwa dawa kila siku.
iv. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo:-
   i. Kufuga kucha wala kupaka rangi za kucha.
   ii. Kunyoa vipara au mitindo ya kihuni.
   iii. Kufuga ndevu.
   iv. Kupaka madawa ya kuchubua ngozi, kupaka wanja, rangi za midomo, manukato au kutumia madawa ya kubadili nywele.
   v. Kuvaa mapambo kama wigi, hereini, mikufu, pete, shanga, bangili, kidani, kipini n.k
   vi. Kutoga masikio au pua.
   vii. Kujichora au kujiwekea alama yoyote katika mwilini mwake.
v. Ni marufuku kuchafua mazingira kwa makusudi mafano kutupa karatasi ovyo, kuchafua vyoo au kupaka vinyesi kuta za vyoo au kujisaidia pembeni mwa tundu la choo.
vi. Ni lazima mwanafunzi asafishe majengo na mazingira na kuyatunza kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

F. UTUNZAJI WA MALI YA UMMA:

a. Ni marufuku kuchora au kuandika kwenye madawati, viti, kuta au vitabu vya kusoma.
b. Vitu vinavyoweza kuhamishika mfano meza, kiti, kabati, n.k visivutwe bali vinyanyuliwe kama itabidi kuhamisha kutoka sehemu moja kwenda nyingine.
c. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika ubaoni bila idhini ya mwalimu.
d. Ni marufuku kuandika maneno machafu mahali popote katika majengo ya shule ndani na nje.
e. Mwanafunzi akiharibu au kupoteza kifaa cha shule lazima afidie au alipe.

G. MIPAKA YA SHULE:

i. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya eneo la shule siku za masomo bila kibali toka shuleni.
ii. Mwanafunzi anapokuwa nje darasa saa za masomo mfano wakati wa mapumziko, asiende nje ya eneo la shule.
iii. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea katika sehemu zifuatazo [illegible] kibali maalum:-